# Dhima za Utanzia katika Riwaya za Kiswahili Mifano Kutoka Kuli na Vuta N'kuvute

**Haji Khatibu Ali**[1]

Swahibaali@ gmail.com

- **Abstract**

**The Roles of Tragic in Swahili Novels**

**Exampels from Dockworker and Tug of War**

Everything under the sun should have specific functions here and there. The field of literature as a sociology discipline does not avoid the threshold of having a responsibility in society. In the long list of literary responsibilities among them are educating, entertaining, promoting language, maintaining and inheriting the deeds of society. In order for the author to master literary work in terms of content, he has to enforce himself to use the elements of form through various artistic techniques. Tragic is the one of artistic elements that are used by literary composers for specific role. The troubling issue is the lack of recognition of his roles in the field of Swahili novels. This flaw is caused by the objection of not being properly addressed by the paper literary stakeholders. This idea is essence of article which is based on a discussion about tragic roles in Swahili novels with reference to *Kuli* (*Dockworker*) and *Vuta N'kuvute* (*Tug of War*). Library reading and interview methods have been fully used in data collection. Data that has been analyzed with descriptive approach guided by functional theory. The paper has revealed that Adam Shafi did not leave it in the air, but he has refined it for eleven basic roles.

**Keywords:** Swahili Novels, Adam Shafi, *Kuli* (*Dockworker*) and *Vuta N'kuvute* (*Tug of War*).

---

(1) PhD student, The State University of Zanzibar (SUZA).

- **Ikisiri**

Kila kilichomo chini ya jua hakijiweki chonjo na dhima za hapa na pale. Uwanja wa fasihi kama taaluma ya sosholojia haikwepi kizingiti cha kuwa na dhima katika jamii. Katika orodha ndefu ya dhima za fasihi miongoni mwazo ni pamoja na kuelimisha, kuburudisha, kukuza lugha, kutunza na kurithisha amali za jamii. Ili mtunzi aimudu vyema kazi ya fasihi kimaudhui hana budi kujilazimisha katika usukaji wa vipengele vya kifani kupitia mbinu mbalimbali za kibunulizi. Utanzia nao ni mojawapo ya kipengele cha kibunulizi ambacho kinatumiwa na watunzi kwa dhima maalumu. Suala linalotatiza ni kutojulikana kwa dhima zake katika ulingo wa riwaya za Kiswahili. Dosari hii inasababishwa na kipingamizi cha kutoshughulikiwa ipasavyo na wadau wa fasihi kiutafiti. Fikra hii ndiyo kiini cha makala hii ambayo imejikita kwenye mjadala unaohusu dhima za utanzia katika riwaya za Kiswahili, kwa kurejelea *Kuli* na *Vuta N'kuvute*. Njia za usomaji wa maktabani na mahojiano zimetumika kikamilifu katika ukusanyaji wa data. Data amabazo zimechambuliwa kwa mkabala wa maelezo huku tukiongozwa na Nadharia ya Uamilifu. Utafiti umebaini kuwa Adam Shafi hakuuacha utanzia hewani, bali ameusarifu kwa madhumuni kumi na moja ya msingi.

## 1.0Utangulizi

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) dhima ya fasihi iwe simulizi au andishi katika jamii hufanana isipokuwa hutofautiana katika vipengele vya utunzi, uwasilishaji, mazingira ya uwasilishaji, hadhira, umri, umilikaji, tanzu, lugha, kubadilika, wahusika, marekebisho na uhifadhi. Katika mlolongo mrefu wa vipengele viwezavyo kutofautiana kidhima ni hiki cha utunzi ambacho kinawafikiana na dhana muhimu ya utanzia. Akifafanua mawazo juu ya utanzia, Ponera (2014: 20 – 21) anadai kuwa ni mbinu ambayo mtunzi hutumia vipengele mbalimbali vizuavyo huzuni, masikitiko, jitimai na mateso kwa hadhira yake. Anaongezea kueleza kuwa vipengele hivyo huweza kujengwa na mateso, ugumu wa maisha, vifungo, mabaa kama njaa, gharika, kimbunga, magonjwa, ulemavu wa viungo au michakato ya mwili, pamoja na ule wa mifumo ya mwili kama vile ugumba, utasa. Mawazo sawa na haya ni ya Ali (2015:5) anayetongoa kuwa, utanzia una maana ya maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye kuifanya hadhira ihuzunike. Anaenda mbali zaidi, tumeitofautisha dhana ya utanzia na tanzia kwa hoja kuwa: Tanzia hujiegemeza katika suala la utendaji, hususani matendo ya jukwaani. Upande wa utanzia ni mbinu inayojengwa kwa misingi ya kuibua majonzi, masikitiko, jitimai na huzuni. Maelezo haya yanasadifu maoni ya Said na Taib (2019:73) pale wanaposema kwamba utanzia ni hali ya kutokea matukio katika kazi ya kifasihi na matukio hayo yakamletea shida, hofu, mashaka, woga na masikitiko msomaji wa kazi husika.

Duru za wataalamu zinaarifu ukweli kuwa dhana ya utanzia ina ukaribu mkubwa na hisia zenye kuhuzunisha, kuhofisha na kuhurumisha. Ukweli wa fikra hizi unaweza kuthibitishwa tunapomakinikia dhima za utanzia kwa hadhira ya wasomaji. Kilicho bayana ni kwamba, riwaya za mwandishi Adam Shafi zimesadifu katika kutumia utanzia, unaoibuka kutokana na ujenzi wa matukio yenye upatanifu na mtiririko mzuri. Kuna vichocheo vingi ambavyo vinaweza kusababisha utokeaji wa utanzia kwa madhumuni mbalimbali ya mtunzi. Kwa mwelekeo wa makala hii,

imedhamiria kuuchunguza utanzia kwa maana ya utokeaji wake kidhima kama ilivyokusudiwa na baadhi ya riwaya za Adam Shafi.

### 1.1 Riwaya ya Kuli kwa Muhtasari

Riwaya ya *Kuli* ilichapishwa mwaka 1979 na kampuni ya *Tanzania Publishing House*. Ni riwaya ya kihistoria kwa sababu inaeleza matukio mbalimbali yaliyojiri visiwani Zanzibar kabla ya Mapinduzi[1]. Kikamusi, Kuli ni mtu anayefanya kazi ya kubeba, kupakia na kupakua mizigo bandarini au stesheni (Mdee na Wenzake, 2011: 248). Katika uwanja wa kifasihi, *Kuli* ni hadithi inayohusu vuguvugu la Wazanzibari kupitia makuli kudai uhuru wa kisiasa, kiuchumi na kijamii dhidi wakoloni. Kwa mujibu wa riwaya hii, Kuli amesawiriwa kama mtu mwenye kuwakilisha tabaka la chini lenye watu weusi, masikini na wasioelimika. Aidha, ni tapo lenye kudhalilishwa kwa kufanya kazi ngumu bila kupata malipo, posho au marupurupu yanayoendana na kazi. Hatimaye, huambulia mateso, vipigo na manyanyaso mengine kutoka kwa mabepari wakisaidiwa na utawala wa Kisultani. Kwa upande mwingine, riwaya inaonesha mikakati kabambe ya mwamko wa kudai mageuzi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Natija ilionekana baada ya kuongezeka kwa mikutano, migomo na maandamano ya nchi nzima. Kila Mzanzibari alitoa mchango wake ili kuhakikisha watawala wanang'atuka nchini Zanzibar.

[1] Katikati ya usiku wa Januari 11-12, 1964, watu wapatao 300 wenye silaha walivamia makao makuu ya Polisi Ziwani na kituo cha Polisi cha Mtoni mjini Zanzibar na kukamata silaha tatu. Kundi la pili la wanaume lilikuwa na jukumu la kukalia kituo cha redio Zanzibar kwa nia ya kukata mawasiliano kati ya visiwa hivyo na dunia nzima. Ndani ya saa chache, iliupindua Usultani wa Zanzibar na serikali yake ya kwanza huru, mwezi mmoja tu baada uhuru wake kutoka Waingereza tarehe 10 Disemba 1963. Sultan Jamshed Abdullah alifanikiwa kutoroka na family yake. Lakini wajumbe wote wa serikali walikamatwa, miongoni mwao ni Waziri Mkuu, Mohammed Shamte, na Waziri wake wa Mambo ya Nje, Ali Muhsin Barwani. Januari 12, 1964, Jamhuri ya watu wa Zanzibar ilianzishwa chini ya uongozi wa Abeid Aman Karume (Fouéré, 2012: 2-3).

Mwisho wa riwaya inazungumziwa kuhusu mfumo wa mahakama kwa namna ambavyo hautendi haki katika kusikiliza na kuhukumu kesi. Mwandishi anaicheka na kuikebehi mahakama kuwa ni sehemu ya kukandamiza haki za wanyonge hususani tabaka tawaliwa.

### 1.2 Riwaya ya Vuta N'kuvute kwa Muhtasari

Riwaya ya *Vuta N'kuvute* inayochukua mkondo wa kihistoria katika awamu ya mwisho ya ukoloni nchini Zanzibari. Pamoja na mambo mengine mengi yanayojadiliwa katika riwaya hii, ni kujipambanua katika kuizungumzia kwa kina asasi muhimu ya ndoa[1]. Katika mrengo huu, ndoa inachukuliwa kama chombo cha kuwakandamiza wanawake wa Uswahilini. Ndoa ambayo inamweka mwanamke kama bidhaa na huku ikimpa uwezo mkubwa mwanamume anayefanya atakalo dhidi yake. Haya yamesawiriwa kupitia ndoa ya Bwana Raza na Yasmin (Uk, 1) pamoja na ndoa ya Yasmin na Shihab (Uk, 175). Pia, riwaya inazungumzia asasi muhimu ya utangamano wa umma. Kwa miongo kadha Zanzibar imekuwa na mseto wa jamii tofauti wakiwamo Waarabu, Waafrika (Washirazi, Wangazija) na Wahindi. Umseto huu ulisababisha ubaguzi wa kiuchumi na kirangi (Constantin, 1989). Katika mikakati ya kukata mizizi ya kibaguzi, riwaya inaonesha mashirikiano ya kijamii bila ya kujali rangi, kabila, dini na hata jinsia. Haya yanasawiriwa kwenye utangamano wa Wahindi na Waswahili. Mfano ni ule wa ukuruba baina ya Yasmin na Mwajuma (Uk, 44). Hata hivyo, riwaya inazungumzia juu ya harakati za Wazanzibari kutafuta ukombozi kutoka kwa wakoloni. Harakati ambazo zimekitwa na vijana dhidi ya Serikali ya Bwana Sayyid chini ya himaya ya Mwingereza (Uk, 64).

[1]Ni makubaliano kati ya mwanamume na mwanamke kuwa na uhusiano wa kudumu kama mume na mke. Uhusiano huu unaweza kuwashirikisha watu wa ukoo katika uteuzi wa mchumba au wanaotaka kuoa na kuolewa kuchaguana wao wenyewe. Ndoa ni ukamilifu wa makubaliano ya muungano wa mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kuwa ni mume na mke kulingana na sheria, mila, au desturi za sehemu fulani (Maitaria, 2012:15).

## 2.0 Mwega wa Nadharia

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Uamilifu. Nadharia hii iliasisiwa na Auguste Comte (1787-1837), Herber Spenser (1830-1903), Wilfredo (1847-1923) na Emile Dukhein (1888-1919) na kuendelezwa na Radcliffe Brown (1881-1955) na Malinowsky (1884-1942) (Taz, Wallace na Wolf, 1980). Bascom (1954:333) anaeleza kuwa vipengele vya fani katika utanzu wowote wa fasihi huweza kutumiwa katika mazingira tofauti kwa lengo la kutekeleza dhima tofauti vilevile. Nadharia hii inatilia mkazo kuchambua dhima zinazojitokeza katika kazi ya fasihi. Inaamini kuwa kila kipengele cha kazi ya fasihi kina maana na hutekeleza jukumu maalumu. Kwa mwegamo wa Nadharia hii, inaonekana kwamba mbinu zitumikazo katika kubuni fasihi huwa na majukumu mahususi. Ukweli huu umo pia kwenye matumizi ya utanzia kama mojawapo ya mbinu hizo na kwamba itakuwa na dhima inapodhihiri ndani ya fasihi. Hivyo basi, Nadharia ya Uamilifu imefaa katika uchambuzi wa makala hii, kwa sababu ilitusaidia sana katika kazi ya kubainisha na kuchambua dhima za utanzia katika riwaya teule za Adam Shafi.

## 3.0 Mbinu za Utafiti na Uchambuzi wa Data

Utafiti ulioizaa makala hii umetumia njia mbili katika ukusanyaji wa data. Ya kwanza ni njia ya usomaji wa maktabani. Kwa kutumia njia hii, tulisoma riwaya za *Kuli* (1979) na *Vuta N'kuvute* (1998) ambazo zimesaidia kubaini na kunukuu maeneo yenye utanzia pamoja na kugundua dhima zake. Njia ya pili iliyotumika ni mahojiano. Kwa hakika mahojiano yalifanywa kwa wabobevu wa fasihi ambao waliwezesha kupata taarifa za moja kwa moja zihusianazo na dhima za utanzia katika riwaya. Katika hatua yingine, mkabala wa kimaelezo ulitumika ipasavyo katika uchambuzi wa data zilizotokana na usomaji wa maktabani na mahojiano.

## 4.0 Dhima za Utanzia katika Riwaya za Kiswahili

Suala la matumizi ya utanzia katika riwaya ya Kiswahili ni la kawaida na lenye kupewa kipaombele na watunzi mbalimbali.

Watunzi huutumia utanzia kama njia mojawapo ya kupaza sauti zao mbele ya jamii husika. Cha mno ni kujiuuliza utokeaji wa utanzia unaofanywa na watunzi una dhima gani katika matini au kwa wasomaji. Usakaji wa majibu ya suali hilo ni wa lazima kwa shabaha ya kuwashibisha wenye kutatizwa na kizungumkuti hiki. Juu ya hili makala imebaini dhima za msingi za utanzia katika maeneo yafuatayo:

### 4.1 Kuihuzunisha hadhira ya Wasomaji

Uandishi wenye kutumia utanzia umekuwa na msaada mkubwa katika kuwajengea huzuni wasomaji. Kadiri ambavyo mtunzi anapoyapa uzito matukio ya kitanzia yenye sura kama ya ugumba na utasa, vifo, magonjwa, mabalaa na mateso ndivyo msomaji huchochewa katika hali ya kutawaliwa na huzuni kiasi ya kumfanya awe mnyonge. Kwa muktadha huo, uandishi unafikia kilele cha kuipa kisogo hadhira katika hali ya kuwa na furaha, kicheko, uchangamfu au tabasamu (Ponera, 2014). Kwa mfano katika riwaya ya *Kuli* mwandishi anaeleza ifuatavyo:

> Majaliwa alikuwa na mkewe aliyeitwa Mashavu. Ijapokuwa Majaliwa na Bi Mashavu walioana walipokuwa vijana, kwa muda mrefu walikuwa hawakubahatika kupata mtoto. Walikata tamaa ya kupata mtoto na hakuna mzimu walioubakisha tokea Unguja hadi Pemba katika jitihada za kuomba mtoto… (Uk, 1).

Tukio jengine ni kupitia riwaya ya *Vuta Nkuvute* ambalo linaweka wazi juu ya msiba uliompata Yasmini. Mwandishi anasema:

> Alilikumbatia gazeti akajifunika nalo usoni akilalamika. “Denge nipe pole! Denge nipe pole!” Aliruka pale alipokuwa amekaa akamkumbatia Denge, kichwa chake amekilaza juu ya bega la Denge, akilia na kulalamika. “Mume wangu! Masikini Shihab!” Furaha na starehe yote iliyokuwemo ndani ya chumba kile

> ikayeyuka chumba kikajaa majonzi (Uk, 194-195).

Kinajitokeza katika mkasa wa kwanza na wa pili ni kutandawaa kwa huzuni na kuyeyuka kwa furaha. Kitendo cha ndoa ya Majaliwa na Mashavu kukosekana mtoto kwa miongo kadhaa, ni mkasa uliowafanya kujawa na majonzi na kukata tama ya maisha. Aidha, mkasa wa Yasmini kufiwa na mumewe aliyempenda ulimuweka na kumbakisha si yeye tu katika simanzi bali hata rafika zake kama Denge na Shihab. Haya yote yanajiri kwa sababu mtunzi alilenga kuwaingiza wasomaji wake katika dimbwi la huzuni.

## 4.2 Kuibusha Maudhui za Mtunzi

Wataalamu wengi wanaafikiana kwamba uga wa fasihi ni sharti utazamwe katika kipengele cha fani na maudhui. Wakizungumzia kuhusu maudhui, Njogu na Chimerah (1999) wanafafanua kuwa, ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi iwe riwaya, tamthilia, shairi au wimbo. Wakiendelea kuvitaja vipengele vijengavyo maudhui ni pamoja na dhamira migogoro, ujumbe, falsafa, msimamo na mtazamo wa mwandishi. Imebainika kuwa uchimuzi wa utanzia katika riwaya upo kwa shabaha ya kuifanya hadhira isalimu amri katika kupokea ujumbe maalumu. Ukweli huu unatiwa nguvu na maoni ya Profesa Wael[1] anayeeleza kwamba:

> Kazi ya kifasihi hujengwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa zinazoafikiana na lengo pamoja na aina ya kazi ya kifasihi inayowasilishwa. Kwa mfano mbinu hii ya utanzia na mbinu nyingine inamchochea

[1] Maelezo haya yalitolewa na Profesa Wael Nabil Ibrahim ambaye ni Muhadhiri wa Fasihi ya Kiswahili na Mwenyekiti wa Idara ya Lugha na Ufasiri ya Chuo Kikuu cha Al – Azahar Misri, katika mahojiano na mtafiti ya Mei 25, 2023.

> msomaji kujitafutia mengi kwa kufumbua ujumbe uliomo katika kazi inayosomwa.

Hii ina maana kuwa umaarufu wa utanzia katika riwaya za Kiswahili hautokani tu kwa maneno au kauli za hapa na pale, bali pia kupitia kwa namna ujumbe unavyowasilishwa na jinsi unavyoakisi hali halisi ya maisha ya watu. Kwa kutumia riwaya ya *Kuli* na *Vuta Nkuvute* matukio yafuatayo yanaleta ujumbe maalumu

> …Kila rungu alilopigwa lilimletea maumivu zaidi kuliko lile alilopigwa hapo awali. Damu ilizidi kuwa nyingi mpaka shati likaloa chapachapa. Damu nyingine iliwarukia wale askari. Harufu ya damu ilianza kumlevya Rashidi na mara alijiona anarembuka huku askari wakiwa na uhuru wa kutosha wa kumtandika marungu mengi zaidi. Mwisho Rashidi alizidiwa na kipigo mpaka akapotelewa na fahamu kabisa. (Kuli:165).
>
> Alisikia mtu akipiga mayowe na kulalamika, “Nakufa! Mnaniua! Mama yangu wee!”… Mlinzi mmoja alimpiga teke la kiuno, mwengine akamkanyaga shingoni, mwengine akamtandika rungu tumboni. Mfungwa yule alipiga kelele mpaka nguvu zikamwisha akabaki kukoroma kama anayekata roho. Aliburutwa kama mzoga akapelekwa upande wa pili wa gereza (Vuta N’kuvute: 208).

Kutokana na madondoo hayo kugusia matukio yenye mwelekeo wa kitanzia katika hali ya utesaji. Yakizingatiwa kwa umakini matukio hayo, yanakidhi sifa ya kuibusha ujumbe maalumu ndani yake. Kwa mfano, ujumbe mama unaopatikana katika mazingira haya ni matumizi makubwa ya nguvu zitokazo kwenye vyombo vya dola. Vyombo hasa vinavyolengwa hapa ni mamlaka za Polisi na Askari wa magerezani. Kwa ujumla, ni vyombo vinavyotoa

taswira ya kukithirisha ukandamizaji dhidi ya wananchi wanyonge. Matarajio ya mwandishi mbele ya hadhira ni kuchukua hatua stahiki na ifaayo katika kudhoofisha uonevu wa vyombo vya dola unaonyima nafasi ya kuchipuza haki za binadamu.

## 4.3 Kuvuta Hisia za Msomaji

Usanii wenyewe upo kwenye kuchukua mguso, taathira na hisia kwa ajili ya kuyachokora yale yaliyomo ndani ya msomaji (Indede, 2011). Katika uhalisi huu, nia za watunzi katika bunulizi zao zipo kwa ajili ya kuzitekenya akili na fikra za hadhira kiundani. Mtekenyo huo hufikia kilele cha kuwatoa wasomaji kutoka ulimwengu wa kidunia na kuwatumbukiza ndani ya ulimwengu wa kisanaa. Makala imebaini kuwa mtunzi hutumia utanzia kuchochea hisia hasi tofauti ambazo huchangia kumteka msomaji akilini, moyoni na mwilini. Hata hivyo, imegundulika katika muktadha wa kuyapiga darubini masuala ya mazishi, vifo, misiba au mauaji yameathiri sana mielekeo na mihemko ya wasomaji kwa kujawa na hofu, huruma, kuchukizwa, kuudhika, kukata tamaa na wasiwasi. Suala hili linaungwa mkono na Dkt Khamis[1] anayedokeza kuwa:

> Adam Shafi ameusana utanzia ili kuvuta hisia za wasomaji. Matukio ya shida na taabu wazipatazo wahusika msomaji hujiona ni sehemu ya ile hadithi. Kwa sababu ni matukio ambayo yamechorwa katika uhalisia wake kama jamii inavyokumbana nayo kila siku.

Tukizigeukia riwaya teule, bila ya ajizi mwandishi anaoneka wazi wazi azma yake ya kuzitekenya hadi kuziathiri hisia za wasomaji kama asimuliavyo:

> Bakari alipogeuka upande wa pili kutaka kumsukuma askari aliyetaka kumvuta mguu,

[1] Mahojiano ya Mei 29, 2023 baina ya mtafiti na Dkt. Tatu Yussuf Khamisi ambaye ni Muhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma katika Taaluma za Kiswahili.

> alipigwa risasi ya kifua na askari mwingine aliyekuwa amejibanza kichochoroni kwa mbali kidogo. Aliruka juu na alipoanguka alifikia juu ya mikono ya Faraji. Alipapatika na haikuchukua muda alinyoka sawasawa na kukata roho. (Kuli:184).

> Walipita kwenye miamba ya mawe, wakaingia kwenye vidimbwi vya maji ya chumvi yaliyomchonyota kwenye vidonda vyake akatamani akae tena kuyauguza maumivu ya miguu yake lakini maumivu ya teke la yule askari aliyahisi mpaka hivi sasa, akaogopa kukaa akichelea asije kupigwa teke jingine… (Vuta Nkuvute: 238).

Katika riwaya ya *Kuli*, ni aibu na fedheha ya hali ya juu kwenye tukio la askari kufanya mauaji ya mwananchi ambaye hana silaha yoyote. Hali kama hii, matokeo yake imevuta kwa karibu hisia ya msomaji kujawa na huruma na woga. Katika hatua nyingine, riwaya ya *Vuta N'kuvute* inaliswairi tukio la maumivu makali wayapatayo mahabusu huku wakiwa katika uchovu na shida ya kutembea umbali mrefu. Ni katika hali ambayo imebainika kuwa imeweza kumwambikiza msomaji kujihisi kutoneshwa na maumivu kama ambavyo yaliwapata mahabusu riwayani.

## 4.4 Nyenzo ya Kujenga Taharuki

Dhima nyingine ya utanzia ni kujenga taharuki kwa wasomaji. Inaelezwa kuwa taharuki ni kipengele kitoacho msisimuko wa msomaji kuwa na shauku na hamu ya kutaka kujua mambo ya mbeleni ndani ya kazi za kifasihi, kiasi ambacho humwezesha kuendelea kufuatilia kisa au hadithi husika. Aidha, ni hisia za wasiwasi au msisimuko alionao mtu anapohisi kuwa jambo fulani litatokea au mtu anapoeleza habari fulani (Hornby, 2014:1209). Imebainika kwamba mojawapo ya kipengele kinachoichochea taharuki kuzuka riwayani ni kutokana na matumzi ya utanzia. Dkt

Moh'd[1] alipoulizwa kuhusu dhima za utanzia katika riwaya za Kiswahili, majibu yake yalikuwa haya yafuatayo:

> Utanzia ni kama mbinu ya ujenzi wa taharuki. Adam Shafi amefanya hivyo si vyengine ili kuwavutia wasomaji wake waweze kufuatilia kwa ukaribu visa na mtiririko wake namna unavyokwenda. Kwa sababu pamoja na kuwepo kwa mbinu nyingi katika fasihi, utanzia unaonekana ni mbinu mwafaka inayosadifu zaidi kwenye taharuki

Zikirejelewa riwaya teule za mwandishi Adam Shafi ni dhahiri shahiri hakuwa mbali na hoja iliyofafanuliwa na mtoataarifa mtajwa hapo juu. Kwa mfano mwandishi anatufumbua macho pale asemapo kuwa:

> "Rashidi kakamatwa," Faraji alijibu kwa sauti ya unyonge. Amina alimtazama Faraji kwa macho makali kama kutaka kumfahamisha kwamba yeye ndiye aliyemtakia yale. Macho yake yalianza kuelea ndani ya machozi na mara machozi hayo yakaanza kumiminika taratibu na kutambaa juu ya mashavu yake. Hapo tena Amina hakuweza kujizuia, alianza kupiga mayowe, "Masikini mume wangu! N' na nini mimi tena! Ameniacha katika hali hii ya uja uzito! Masikini mume wangu! Masikini mume wangu!... (Kuli: 166 – 167).

> Kama hukuweza kuishi na Raza basi na sisi hatuna pa kukuweka," mjomba wake Yasmini alisema kwa kelele. Kelele zilikuwa kubwa mpaka majirani wakaanza kuchungulia madirishani. "Tena upesi tuondokee mbele ya

[1] Ni Dkt Masoud Nassor Moh'd ni Muhadhiri Mwandamizi wa Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Mahojiano yaliyofanyika Mei 10, 2023 kwa njia ya mtandaoni.

> macho yetu utafute pa kwenda. Toka!" alifoka mjomba. Yasmini alisita kidogo na kumtazama mjomba wake, matone ya machozi yakianza kuteleza taratibu kutoka kwenye macho yake mazuri. "Nakwambia toka! Nenda zako! Nenda kamtafute huyo unayempenda." "Niondoke nende wapi na hapa ndiyo kwetu?" alisema Yasmini kwa unyonge… (Vuta N'kuvute:16).

Bila ya shaka matukio yote yaliyomo kwenye *Kuli* na *Vuta N'kuvute* yanamraghibisha msomaji kiu ya kutaka kufahamu nini kitatokea usoni. Katika *Kuli* kunasawiriwa tukio la Rashidi kukamatwa na polisi lakini pia kuna tukio la Amina kusononeka akiwa katika kilio kwa kuachwa na hali ya ujauzito. Kwa upande wa *Vuta N'kuvute* kunachorwa tukio la Yasmin kufukuzwa kwao na kutokujua wapi atafikia kimakaazi. Matukio yote haya yamebainika kuwa yanasisimua na yamejengwa kama turufu ya mtunzi katika kuiweka hadhira yake kwenye taharuki ya kuendelea kuvisoma vitabu ili kujua kianchokea baadaye.

## 4.5 Kusawiri Uhalisia wa Kiubunifu

Riwaya ina sifa ya kuzungumzia masuala nyeti ambapo mtunzi huchora wahusika wake kwa ustadi mwingi huku akionesha jinsi wanavyotagusana na mazingira halisi. Mazingira halisi hutokana na urejeleaji wa maisha ya kawaida yanayotokea kila siku ambapo mtunzi huyatazama na kuyahusisha na majina ya wahusika, kusema, kula na kuvaa kwao (Mbatiah 2001: 71; Madumulla 2009: 5). Hii ni kwa sababu fasihi haitokei katika ombwe tupu bali hudhihirisha hali ya maisha ya wanajamii katika nyakati na mazingira yanayobadilika kutokana na mifumo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia. Hayo yote yanajiri kwa kuwa mtunzi huiga shughuli za binadamu katika jamii na hatimaye kuzisawiri katika kazi ya sanaa kwa kuzingatia mbinu faafu za ubunaji (Okal, 2021:15). Kwa maoni yetu utanzia ni mojawapo ya mbinu kindakindaki yenye kubuniwa kuendana na yale yatokeayo

ndani ya jamii husika. Ufafanuzi wa Dkt Mganga[1] unaarifu kwamba:

> Jambo kubwa linalomfanya Adam Shafi kutumia utanzia ni kuonesha uhalisia. Hii ni kwa sababu maisha yana pande mbili ambazo ni furaha na huzuni. Kwa maana mwandishi hawezi kuzungumzia furaha tupu au huzuni tupu. Lazima azungumzie pande moja ambayo yeye anaona imemgusa zaidi ili kuihalisisha kazi yake na jamii. Na kufanya hivyo kunatokana na mambo yenye kuhuzunisha ndiyo yenye kuitatiza jamii.

Kutokana na kauli hii imebainika kwamba, riwaya za *Kuli* na *Vuta N'kuvute* zimekuwa mstari wa mbele katika kuyamurika matendo ya wahusika kama yalivyojitokeza katika jamii ya Wazanzibari. Ikikumbukwa kuwa riwaya zote mbili zina mwelekeo wa kihistoria ambazo zimezungumzia sira ya Zanzibari katika hekaheka za kutafuta ukombozi wa kisiasa, kijamii na kuchumi. Humo mwandishi ameyabainisha masuala yaliyoviza furaha kama wananchi kukabiliwa na vifungo, mateso, masimango, vitisho kutoka kwa watawala wa kigeni. Kwa mfano ukurasa wa 51 katika *Kuli*, Rashidi anafukuzwa kazi na Morarji kutokana na kudai nyongeza ya mshahara. Pia, ukurasa wa 170 katika *Vuta N'kuvute* yanasawiriwa madhila ya vipigo alivyovipata Denge kutoka kwa Inspekta Wright. Haya yote yanajiri kwa lengo la kuakisi uhalisia uliombatanishwa na kudai uhuru ambao ni vigumu kupatikana kwa furaha na kiulaini.

## 4.6 Kuwafariji Wasomaji

Kwa pamoja Wamitila (2003) na Herman (2011) wakizungumzia kuhusu dhima ya utokeaji wa faraja katika fasihi,

[1] Ni Dkt Nawaje Ali Mganga ni Muhadhiri wa Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al - Sumait. Ambaye pia ni Mudiri wa Idara ya Lugha chuoni hapo. Ni katika mahojiano yaliyofanyika Mei 27, 2023 kwa njia ya mtandaoni.

wanakiri kuwa hutokea hasa pale panapokuwa na suala la kusikitisha au hisia za majonzi. Kupitia safu hii, uchunguzi uliofanywa na utafiti imebainika kwamba utanzia hupambaza akili na kiwiliwili cha msomaji. Huku ikisaidiwa na uingizaji wa vilio, maombolezi, lugha ya kuhuzunisha na lugha ya upole. Matokeo yake huwajengea wigo mpana wasomaji kuambaa kizingiti cha kufarajika. Kwa maneno mepesi, utanzia ni kama njia ya kuipumzisha hadhira kutokana na madhila na changamoto zinazowakumba wahusika. Ili kuweza kufahamu kiundani suala hili, Bw. Haji[1] ana maoni haya:

> Utanzia unajengwa kutokana na matatizo mbalimbali katika jamii. Nao waandishi wa Kiswahili hawapitwi na fursa ya kuwaliwaza wasomaji kwa njia ya kuyatumia matukio hayohayo yanayowaumiza wahusika. Mwandishi huweza kutumia matukio ya kuhuzunisha kama kiliwazo hasa pale muhusika anaposalimika kutokana na dhiki alizobebeshwa.

Suala la utanzia kutia faraja kwa wasomaji unadhihirika katika baadhi ya maeneo ndani ya Riwaya ya *Kuli* na *Vuta N'kuvute*. Kwa mfano katika riwaya ya *Kuli* imegundulika kuwa kitendo cha Rashidi kufukuzwa na Morarji kazi kama mbwa, ni tukio lililoloibusha faraja kwa msomaji baada kuajiriwa sehemu nyingine. Kadhalika, katika *Vuta N'kuvute*, Denge anaingizwa gerezani na kupata mateso ya hapa na pale akiwa katika mazingira hayo. Kama ijulikanavyo gerezani ni sehemu ya kuififisha furaha na uchangamfu. Lakini kupitia humo gerezani ndimo mnapopatikana faraja ya msomaji kwa kutoroshwa katika mpango kabambe ulioandaliwa na Bukheti pamoja na Yasmini.

[1] Mahojiano baina ya mtafiti na Bw. Gora Akida Haji yaliyofanyika Mei 18, 2023. Bw. Gora Akida Haji ni mwanafunzi wa Shahada ya Tatu (Uzamivu) katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

## 4.7 Kuonesha Ustadi wa Kiutunzi

Ustadi ni ujuzi wa kusana jambo kwa uweledi, uhodari, ufundi na hatimaye kuibua ufanisi (BAKITA, 2015:1126). Mara nyingi msanii hutambua kuwa ana wajibu na jukumu kubwa kwa jamii yake na hivyo hujinasibisha kuambatana na vionjo vya kiumbuji ambavyo hukidhiwa kwa kupitia vipengele mahsusi vya kisanaa ndani ya kazi ya fasihi (Senkoro, 1995:89). Inavyoonekana kupitia kauli hii ni kwamba ustadi au uwezo wa msanii unaweza kupimwa na kutathminiwa katika kutumia vyema mbinu tofauti za kisanaa. Mbinu za kisanaa ni ule ufundi ambao unatumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi katika kuijenga kazi yake (Senkoro, 2011). Kama ilivyoelezwa huko nyuma kwamba utanzia ni miongoni mwa mbinu za kisanaa zenye kutoa matokeo ya huzuni, huruma na hofu kwa hadhira. Imebainika kweupe kuwa haikuwa rahisi hata kidogo, Adam Shafi kuwajenga wahusika wake katika mazingira yaliyoja hofu, wasiwasi, huzuni, vilio vyenye machozi na kutawaliwa na huruma baina yao. Ujenzi wa namna hii ulidhamiria pia kuwaambukiza wasomaji. Mtoataarifa mmoja alieleza kuwa:

> Ujenzi wa ufutuhi wenye kusudio la kuwafurahisha wasomaji ni rahisi mno kuliko ujenzi wa utanzia unaolenga kuihuzunisha hadhira. Kuifanya hadhira mpaka ilie, iny'ong'onyee, ikate tamaa, iwe nyonge si kazi nyepesi. Kufanya hivyo, hakuji burebure tu, bali kuna nguvu fulani ya uhodari aliyokuwa nao mtunzi. Na utaona hata katika runinga kuna vipindi vyingi vilengavyo kuchekesha lakini hukuti vipindi vinavyoendesha kipindi cha kuwaliza watazamaji.

Suala hili halikufumbiwa macho na Adam Shafi hasa pale alipoonesha ustadi mkubwa wa kuwatengeneza wahusika wake katika hali ya kuwaliza. Kwa mfano, katika *Kuli* ukurasa wa 98 inasimuliwa kadhia ya Rashid kulia kama mtoto mdogo baada ya kuondokewa na mama yake mpenzi, mama aliyempatia tabu uhai

wake wote. Inasimuliwa pia namna ya majirani hawakuacha kumbembeleza na kumliwaza huku wakimsaidia katika kilio. Katika kiwango hikihiki, *Vuta N'kuvute* ukurasa wa 128, Yasmin anachorwa kwa namna ambayo anatoa vitone vya machozi kutokana na kujawa na huruma dhidi ya Denge.

### 4.8 Kukuzisha Umakini na Kumbukumbu kwa Msomaji

Utanzia pia huweza kuwa kiungo muhimu cha kukuza umakini na kumbukumbu katika mwenendo mzima wa visa husika. Hii inatokana na hali ya kushamiri kwa matumizi ya utanzia katika riwaya. Kwa kweli jazaa yake ni kuacha alama katika bongo na fikra za msomaji. Kwa mfano, ni jambo la kawaida mwanadamu kuyakumbuka kiurahisi madhila yakumtayo kuliko yale mazuri yaliyompitikia maishani mwake. Kadhalika, Waswahili mara kwa mara hutolea mfano kwamba mke katika nikahi afanyiwe mazuri mengi lakini siku anayokerwa anayakumbushia maudhi ya nyuma hata kama jambo hilo limepita miaka kumi. Huu ni uyakinifu unaotilia nguvu juu ya mambo yasiyofurahisha yanakaa zaidi akilini. Mtoataarifa mmoja anaongezea kwa kusema kuwa:

> Masuala haya ya kitanzia yanasababisha kutosahaulika. Huwezi kusahau jambo baya kama ambavyo jambo zuri linavyokujia. Kwa hiyo utawakuta wasomaji wanaweza kuyasimulia masuala yale mabaya ambayo hayafurahishi kwa msingi wa walivyoyashuhudia wakati wa utalii wao. Kwa mfano masuala ya mauaji, vifo vya wahusika, majanga wayapatayo wahusika, kudhulumiwa au kunyanyaswa kwao na kadhalika. Na pia isitoshe, hali hiyo humjenga msomaji kuwa na umakini katika mtiririko mzima wa visa na vitushi riwayani.

Ukweli wa mawazo haya yanaweza kuthibitishwa katika baadhi ya visa vya kitanzia katika riwaya hizi teule. Kwa mfano mtoataarifa mmoja alipoulizwa tukio gani lisilofurahisha

unalikumbuka kwa haraka katika riwaya ya *Kuli*? Majibu yake yalikuwa ni ajali iliyotokea bandarini inayomuhusu Kuli ambaye bega na mfupa wake ulidata na kutothaminiwa na watawala wa Kiingereza. Bahati uzuri mtafitiwa huyo aliutaja mpaka ukurasa wake ambao ni wa sita hadi saba. Mtoataarifa mwingine alipoulizwa tukio gani lisilofurahisha wakati wa kusoma *Vuta N'kuvute*? Jibu lake lilikuwa kupigana kati ya Yasmin na Mwajuma ambapo Yasmini alimtafuna Mwajuma ziwa na kumwacha katika hali ya kupiga kelele nyingi kutokana na maumivu makali aliyoyapata. Ugunduzi wetu ulilikuta tukio hili ukurasa wa 152.

## 4.9 Nyenzo ya Kupaza Ujumi

Kuhusu ujumi, duru za wataalamu zinaarifu kuwa ujumi ni taaluma inayoshughulikia uzuri, ubaya, vionjo hasi au chanya, ubora, udhalili na kufaa au kutokufaa. Anaongezea kuwa vigezo vya kupima ujumi ni kama vile utambuzi wa akili, utambuzi wa hisi, utashi wa desturi, uhalisi wa maisha, dhima, umajumui, ulinganisho, utamaduni, uzoefu, ustadi, mwigo na taswira (Badru, 2020:21). Maelezo haya yana mshabihiano na yale ya Wamitila (2008) anayeeleza kuwa hisi, hisia na akili vinategemewa katika kufanya maamuzi ya kiujumi. Kwa kuwa utanzia ni kionjo kiashiriacho masuala yasiyofurahisha, kama ambavyo Mganga[1] (2023) anavyotilia umaanani juu ya kwamba utanzia unajumuisha mambo yote yasiyofurahisha, mambo yote yanayochukiza, mambo yote yanayochefua na yanayomletea machungu msomaji. Ndivyo kionjo hiki kinavyojitanibu kwenye kuihukumu kazi ya kifasihi katika mwondoko wa ubaya. Kutokana na kushamiri kwa matumizi ya utanzia riwayani, imebainika kuwa utanzia ni kiambata kilicho karibu sana na ujumi kutokana na hisia hasi azipatazo msomaji. Kwa mfano vitendo kama vya udhalilishaji, uliaji, ugumba, magonjwa, utesaji, upigaji, uuaji, ufungaji au umahabusu vinawezwa kutambulika kama sehemu ya kuushibisha

[1] Ni Dkt Nawaje Ali Mganga ni Muhadhiri wa Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait katika mahojiano yaliyofanyika Mei 27, 2023 kwa njia ya mtandao.

ujumi. Siyo tu kwamba vitendo hivyo vinaashiria ubaya pekee, bali pia vinamvunjia heshima, utu na thamani ya mwanadamu.

## 4.10 Kutambulisha Mtindo Binafsi wa Mwandishi

Kulingana na Wamitila (2003) mtindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Anajalizia kuwa mtindo hurejelea sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha kwenye fani yake. Maelezo haya yanaungwa mkono na Mulokozi (1989) akieleza kuwa mtindo ni tabia ya utungaji ambayo hupambanua mtunzi mmoja na mwingine. Kuambatana na mawazo ya wanazuoni hawa, imebainika kwamba kadiri utanzia unavyojipenyeza ndani ya kazi fulani ya kifasihi, ndivyo upekee binafsi wa mtunzi unavyodhihirika. Mdhihiriko wa utanzia katika riwaya teule za Adam Shafi umeelemewa sana kwenye uhistoria na kumili katika mazingira ya mahabusu au ufungwani. Kwa mfano, katika riwaya zote mbili wahusika wakuu wamechoreshwa kuonja joto la kukaa gerezani kwa kipindi fulani. Kupitia riwaya ya *Kuli*, tunamuona Rashidi alivyokamatwa na kuwekwa mahabusu kwa muda wa miezi mitatu na ulipoingia mwezi wa nne kesi yake ilianza (Uk, 185). Hata hivyo, Riwaya ya *Vuta N’kuvute* inalisawiri tukio la Denge kuwekwa kizuizini kama mahabusu alionja sulubu za mateso akiwa gerezani (Uk, 237).

## 4.11 Kukwepa Udhibiti Kutoka Mamlaka za Kidola

Akifafanua kuhusu udhibiti ndani ya fasihi, Thiong’o (2003:54) anasema kuwa udhibiti ni kitendo cha kurekebisha umbo, mtindo na maudhui ya mawazo unaotekelezwa na mamlaka ya kidini, au mamlaka za kidunia zenye nguvu ya kuanzisha au kutekeleza hatua za kuadhibu kwa jina la manufaa ya juu yenye kudumisha maadili ya kikundi, jumuiya au taifa. Kama hii haitoshi, Wamitila (2003:249) anadadavua kuwa sifa ya kuyadhibiti maandishi ya kifasihi inayohusishwa na tawala za kimabavu ambazo zinaubana uhuru wa kimaandishi na kusoma. Kusema kweli udhibiti wa kazi za fasihi ni mojawapo ya matatizo yanayowakumba waandishi wengi ulimwenguni. Hali hii hutokea pale ambapo mamlaka

hupiga marufuku kazi za waandishi kusomwa au kutazamwa kwa msingi wa kufanya uchochezi wenye kuzua sokomoko katika jamii. Kwa kutumia mbinu za kisanaa, waandishi huunganisha vyema ubunifu na uhalisia ili kueleza jambo lolote katika hali ya kificho. Bw. Simba[1] alikuwa na maoni yafuatayo katika kukazia nukta hii:

> Sababu kubwa ya kutumia utanzia katika kazi za ni kama mtindo mpya. Kwamba waandishi husema mambo kwa tahadhari ili kukwepa dola wakati wa kufikisha fasihi yao. Aidha, utanzia huu ulikuwa ukitumika kwa mambo ambayo kuyasema waziwazi hayawezekani. Huwa wanaikosoa serikali au taasisi zilizomo nje ya serikali bila kusema ana kwa ana ili isije kuwapatia shida mbeleni.

Kwa kuzingatia yaliyosemwa na wanazuoni hapo juu, pamoja na mambo mengine mengi inayoihusu mbinu hii, imebainika kuwa utanzia kama mojawapo ya mbinu za kisanaa inayotumiwa kwa kutimiza kiu ya kujiweka mbali na vikwazo vitokanavyo na mamlaka za kidola. Mathalani, mwandishi wa *Kuli* na *Vuta N'kuvute* anatumia vilio vya machozi, misiba, maombolezo ya mazishini nakadhalika kama shutuma anazozitoa dhidi ya mfumo dhalimu unaojengwa kwa mgongo wa wakoloni. Katika riwaya zote mbili mtunzi anatumia utawala wa ukoloni kupitia historia ya Zanzibar kama kuwazubaisha watawala wa zama hizi na zijazo. Lakini kiundani anayalenga mamlaka yoyote yenye kusababishia wananchi kuishi kwa shida na mateso ya hapa na pale.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii ilinuia kuchambua na kudadavua uamilifu wa utanzia katika riwaya za Kiswahili. Katika kufanikisha kiu ya azma hii, makala imezitumia riwaya ya *Kuli* na *Vuta N'kuvute*

[1] Simba Haji Gora aliyefanyiwa mahojiano na mtafiti Mei 15, 2023. Bw. Simba Haji Gora ni mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

kama sehemu ya urejelezi wa mifano angavu. Kwa kusaidiwa na mbinu ya usomaji wa maktabani na mahojiano pamoja na Nadharia ya Uamilifu, makala imebaini uwepo wa dhima za kumi na moja za utanzia. Msingi mkubwa wa dhima hizo ni kuihuzunisha hadhira ya wasomaji, kubainisha maudhui za mtunzi, kuvuta hisia za msomaji, nyenzo ya kujenga taharuki, kusawiri uhalisia wa kiubunifu, kuwafariji wasomaji, kuonesha ustadi wa kiutunzi, kukuzisha umakini na kumbukumbu kwa wasomaji, nyenzo ya kupaza ujumi, kutambulisha mtindo binafsi wa mtunzi na kukwepa udhibiti kutoka mamlaka za kidola. Masuala yaliyobainika humu ni kielelezo tosha kuwa fasihi pamoja na tanzu zake na vipera vyake vimo kwenye kufanya kazi maalumu. Kinachorejelewa zaidi hapa ni kuuchukulia utanzia kama kionjo cha kisanaa, chenye ufundi unaoshuhudiwa katika ruwaza maalumu za maneno au matendo yatendwayo na wahusika tofauti riwayani. Lengo lake ni kujenga mnato wa kisanaa katika hali au matukio hayo. Pamoja na mambo mengine, kikubwa kinachouhusu utanzia ni kufanyiwa uchunguzi zaidi ili kugundua mengi yaliyofichama dhidi yake.

## • Marejeleo


- Ali, H.K. (2015). Matumizi ya Utanzia katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed. Tasnifu ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Badru, Z.A. (2020). "Taswira na Mabadiliko ya Kiujumi katika Vitendawili vya Kiswahili". Katika Mulika Na, 39. Uk, 20 – 34.
- Baraza la Kiswahili la Taifa. (2015). Kamusi Kuu ya Kiswahili. Longhorn Publishers Ltd. Nairobi.
- Bascom, W.R. (1954). "Four Functions of Folklore". The Journal of American Folklore. Vol, 67. (266). Pp, 333 – 349.
- Constantin, F. (1989). "Social Stratification on the Swahili Coast: From Race to Class." Journal of the International Africa Institute. Vol, 59. Cambridge University Press.
- Fouéré, M. (2012). "Remembering the Dark Years (1964 – 1975) in Contemporary Zanzibar." The International Journal for the Study of Culture and Society.
- Herman, L. (2011). "Dhima ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili". Katika Kioo cha Lugha. Juz, 9. Uk, 73 – 83.
- Hornby, A. S. (2004). Oxford Advanced Lerner's Dictionary. Oxford University Press. New York.
- Indede, F. (2011). "Mwanamke Angali Tata katika Ushairi wa Kisasa". Katika Swahili Forum. Uk, 163 – 197.
- Madumulla, J.S. (2009). Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi. Mture Educational Publishers. Dar es Salaam.
- Maitaria, N. (2012). Mwongozo wa Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine. Longhorn Publishers Ltd. Nairobi.
- Mbatiah, M. (2001). Kamusi ya Fasihi. Standard Textbooks. Nairobi.
- Mdee, J. S na Wenzake. (2011). Kamusi ya Karne ya 21. Longhorn Publisher Ltd. Nairobi.
- Mulokozi, M.M. (1989). "Tanzu za Fasihi Simulizi". Katika Mulika Na, 21. Uk, 1 – 24.

– _______________ (1996). Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam.
– Njogu, K. & Chimerah, C. (1999). Ufudishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.
– Okal, B.O. (2021). "Uhakiki wa Riwaya ya Paradiso kwa Msingi wa Nadharia ya Uhalisia". Katika Swahili Forum 28. Uk, 14 – 33.
– Ponera, A.S. (2014). Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi. Karljamer Print Technology. Dar es Salaam.
– Said, Z & Taib, A.H. (2019). Fasihi ya Ufungwa Nadharia na Mikabala ya Uhakiki – Riwaya kama Kifani. Heko Publishers. Dar es Salaam.
– Senkoro, F. E.M K. (1995). "E. Kezilahabi: Shaaban Robert wa Pili". Katika Kioo cha Lugha. Juz, 1. Na, 1. Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
– _________________ (2011). Fasihi. KAUTTU Limited. Dar es Salaam.
– Shafi, A. (1979). Kuli. Tanzania Publishing House. Dar es Salaam.
– _________________(1998). Vuta N'kuvute. Mkuki na Nyota. Dar es Salaam.
– Thiong'o, N. (2003). "Licence to Write: Encounters with Sensorship". Katika Comparative Studies of South Asia, Africa and the Middle East. Juz, 23. Na, 1&2. Uk, 54 – 57.
– Wallace, R.A. & Wolf, A. (1980). Contemporary Sociological Theory. Prentice Hall. California.
– Wamitila, K. W. (2003). Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi. Focus Publishers. Nairobi.
– _______________ (2008). Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Vide – Muwa Publishers. Nairobi.